





Kwa nini mbingu ni za rangi ya samawati?



Je, ni samawati kila wakati?



Kwa nini majani ni ya kijani kibichi?




Sio ya kijani kibichi kila wakati.



Kwa nini ndizi ni za njano?



Ndizi mbivu ni za njano.
Ndizi mbichi ni za kijani kibichi.




Kwa nini miavuli ni mieusi?



Miavuli yote si mieusi.



Kwa nini damu ni nyekundu?



Kuna madini kwenye damu.
Yanaifanya damu kuwa nyekundu.



Kwa nini chumvi ni nyeupe?
Sijui!

